TB/LEP 13 A

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Wizara ya Afya

## Mpango wa Taifa wa Kifua Kikuu na Ukoma

# REJESTA YA WANAOHISIWA KUWA NA TB NA UKOMA KATIKA JAMII

Jina la Kituo: ____________________ Halmashauri: ____________________ Mkoa: ____________________

Toleo la 2023

**Rejesta ya wanaohisiwa kuwa na TB na Ukoma katika jamii: TB/LEP 13A**

Rejesta hii inatumika kusajili wahisiwa wote wa ugonjwa wa Kifua Kikuu na Ukoma katika jamii, waliochunguzwa na kuonekana na dalili mojawapo za magonjwa haya. Rejesta hii pia inatunza taarifa za wahisiwa kutoka katika jamii ikiwa ni pamoja na uchunguzi, upimaji na matokeo ya uchunguzi na hatua zilizochukuliwa. Taarifa zinazojazwa kwenye rejesta hii zinatoka kwenye fomu namba TB/LEP 12, Fomu TB/LEP 15, TB/DR TB 03 na LEP 03. Rejesta hii inajazwa na watoa huduma za TB katika jamii (vikundi vya watu waliougua kifua kikuu na kupona, watoa huduma ngazi ya jamii na asasi za kiraia). Rejesta hii huhifadhiwa katika kituo cha kutolea huduma za afya katika jamii husika.

**Hakikisha sehemu zote zinajazwa ipasavyo.**

**NAMNA YA UJAZAJI**

**Jina la kituo:** Andika Jina la kituo ambacho rejesta hii inatunzwa, ama kituo kinachohusika na usimamizi wa kikundi hiki.

**Halmashauri**: Andika Jina la halmashauri taarifa zinakokusanywa

**Mkoa:** Andika Jina la mkoa ambako taarifa zinakokusanywa

**Safu ya (1) Na.:** Andika namba kwa mtiririko ukianzia na namba 1 na kuendelea kila mwanzo wa mwezi.

**Safu ya (2) Tarehe:** Andika siku/mwezi/mwaka wa kusajiliwa kwa mteja katika rejesta hii

**Safu ya (3) Jina la Mteja (Majina matatu):** Andika majina matatu (la kwanza, kati na ukoo) kama mistari inavyoonyesha

**Safu ya (4) Jinsi (Me/Ke):** Andika KE kama ni mwanamke, andika ME kama ni mwanamume

**Safu ya (5) Umri (Miaka):** Andika umri wa mgonjwa kwa miaka kamili. Iwapo mgonjwa ana umri chini ya mwaka mmoja andika sifuri (0)

**Safu ya (6) Namba ya Simu ya Mteja na Mtu wa karibu:** Andika namba ya simu ya mteja msitari wa juu na namba ya mtu wa karibu msitari wa chini.

**Safu ya (7) Mahali Mteja Anapoishi (kitongoji/Kijiji/Mtaa):** Andika kitongoji/Kijiji/mtaa anapoishi mteja

**Safu ya (8) Uchunguzi wa TB au ukoma:** Andika namba 1 kama ni uchunguzi wa TB, andika namba 2 kama ni uchunguzi wa ukoma. Kama atafanyiwa uchunguzi wa magonjwa yote, andika mistari miwili kila uchunguzi wa ugonjwa na mstari wake.

**Safu ya (9) Aina ya mteja au Mahali mteja alipofanyiwa uchunguzi**: Weka au andika namba ambapo mteja alipofanyiwa uchunguzi kama ni;

> **Safu (9) i. Anaishi kaya au karibu na mgonjwa wa TB au ukoma:** Andika namba 1 kama ni **ndiyo** na andika 2 kama ni **hapana**
>
> **Safu (9) ii. Kundi maalum:** Andika namba ya kundi husika ambako mteja ametoka, mfano 1 kama ni Mchimbaji(machimbo/migodi), 2 kama ni mfungwa/Afisa wa magereza, 3 kama ni PWUD na 4 kama ni Mvuvi(kambi za Wavuvi).
>
> **Safu (9) iii. Mkusanyiko wa watu/sehemu nyingine**: Andika namba ya mkusanyiko husika ambako mteja ametoka; mfano 1 kama ni Duka la dawa, 2 kama ni Mganga wa jadi ,3 kama ni Sokioni na 4 kama ni Nyumba ya Ibada.

**Safu ya (10) Aina ya Rufaa:** Andika namba ya aina ya rufaa ambayo mteja amepewa kama ilivyoainishwa kwenye safu hiyo (1. Sampuli; 2. Mteja)

**Safu ya (11) Sababu ya Rufaa:** Andika namba ya sababu ya rufaa ambayo mteja amepewa kama ilivyoainishwa kwenye safu hii (1. Vipimo; 2. Tiba Kinga, 3. Changamoto za Jinsia na haki za binadamu zinazohusiana na huduma ya Kifua Kuu na Ukoma).

**Safu ya (12) Jina la kituo cha huduma za afya rufaa ilikoenda**: Andika jina la kituo cha kutolea huduma za afya alipopelekwa mteja/sampuli kufanyiwa uchunguzi

**Safu ya (13) Aina ya Kipimo:** Andika aina ya kipimo kilichotumika kumchunguza mteja (GeneXpert, Hadubin, Trunati, X-ray, score chart, nyinginezo. Taja)

**Safu ya (14) Matokeo ya rufaa:** Weka alama ya vema (√) katika safu husika kulingana na matokeo ya uchunguzi wa Kifua Kikuu au Ukoma ikiwa TB/DR-TB au Ukoma haujagundulika, TB/Kifua Kikuu kimegundulika, DR-TB/Kifua Kikuu Sugu Kimegundulika, Sampuli haina ubora au Ukoma umegundulika

**Safu ya (15) Amepima VVU:** Weka N kama jibu ni ndio na H kama jibu ni hapana. Usiendike matokea ya vipimo au Hali ya mteja ya VVU.

**Safu ya (16) Ameanza tiba ya TB; DR-TB au Ukoma:** Weka alama ya vema (√) kama ameanza tiba mstari wa juu na namba ya usajili ya TB; DR-TB au Ukoma mstari wa chini.

**Safu ya (17) Matokeo ya matibabu:** Andika matokeo ya matibabu kulingana na rejesta ya kituo cha tiba (TB03; MDR-TB au LEP 03 rejesta) kwa kushirikiana na DOT nesi.

**Safu ya (18) Jina la mtoa rufaa ngazi ya jamii:** Andika majina mawili ya mtoa huduma aliyemfanyia uchunguzi mteja husika na kumpa rufaa kwa usahihi

**Safu ya (19) Maoni/ Maelezo mengine:** Andika maoni au maelekezo mengine mfano jina la asasi na maelezo mengine muhimu

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TB/LEP 13 A**

**Wizara ya Afya**

**Mpango wa Taifa wa Kifua Kikuu na Ukoma**

# REJESTA YA WANAOHISIWA KUWA NA TB NA UKOMA KATIKA JAMII

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | | | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | | | | | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Na | Tarehe | Jina la Mteja (majina matatu) | Jinsi (Me/Ke) | Umri (Miaka) | Namba ya simu ya mteja na mtu wa karibu | Mahali Mteja Anapoishi (Kitongoji/ Mtaa) | Uchunguzi wa TB au ukoma | Aina ya mteja au Mahali alipofanyiwa uchunguzi | | | Aina ya Rufaa: 1. Sampuli 2. Mteja *(weka namba 1 au 2)* | Sababu ya Rufaa | Jina la kituo cha huduma za afya rufaa ilikoenda | Aina ya Kipimo (GeneXpert, Hadubin, Trunati, X-ray, score chart, nyinginezo. Taja) | Matokeo ya rufaa (weka √ panapohusika) | | | | | Amepima VVU *(weka N kama jibu ni ndiyo, H kama ni hapana)* | Ameanza tiba ya TB/ DR TB au ukoma *(weka √ kama ameanza na namba ya TB/DR-TB au ukoma kwa chini)* | Matokeo ya matibabu *kulingana na rejesta ya kituo cha tiba (TB03/DR TB au LEP 03 Register)* | Jina la Mtoa rufaa ngazi ya jamii | Maoni/Maelezo mengine (Jina la Asasi na maelezo mengine) |
| | | | | | | | Andika 1 au 2<br>1. TB<br>2. ukoma | Anaishi Kaya au Karibu na mgonjwa wa TB au ukoma: 1. Ndiyo 2. Hapana *(Andika namba* | Kundi Maalum *Weka namba kutoka kwenye (Kielelezo A)* | Mkusanyiko wa watu/sehemu nyingine *(Weka namba kutoka kwenye Kielelezo B)* | | 1. Vipimo<br>2. Tiba Kinga<br>3. Changamoto za Jinsia na haki za binadamu | | | TB, DR TB au ukoma haujagundulika | TB Kifua Kikuu | DR-TB Kifua Kikuu sugu | Sampuli haina ubora | Amegundulika na ukoma | | | | | |
| 1 | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 2 | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 3 | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 4 | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 5 | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 6 | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 7 | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 8 | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 9 | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 10 | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |

**Kielelezo A:**

1. Mchimbaji (Machimbo/ migodi)
2. Mfungwa/Afisa wa Magereza
3. PWUD
4. Mvuvi (Kambi za Wavuvi)

**Kielelezo B:**

1. Duka la dawa
2. Mganga wa Jadi
3. Sokoni
4. Nyumba ya Ibada
5. Mikutano ya hadhara
6. Shule/Vyuo
7. Kwingineko (Taja)